# TAARIFA YA MHE. HAMZA S. JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWA WAANDISHI WA HABARI JUU YA MAANDALIZI YA UZINDUZI WA KAMATI ZA USHAURI WA KISHERIA NGAZI YA MKOA NA WILAYA TAREHE 16 FEBRUARI, 2026 NA KUFUATIWA NA KLINIKI YA SHERIA BILA MALIPO TAREHE 16 - 22 FEBRUARI KATIKA MKOA WA DAR ES SALAAM.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana siku ya leo kwa ajili ya kuzungumza nanyi kuhusu Uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kamati hizo, kwa wilaya na mkoa wa Dar es Salaam zinatarajiwa kuzinduliwa tarehe **16 Februari, 2026 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja – Dar es Salaam na kufuatiwa na uendeshaji wa Kliniki ya Sheria bila malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa Jirani kuanzia tarehe 16 Februari, 2026 hadi 22 Februari, 2026.**

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Napenda pia kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake na zaidi kwa kulinda, utawala wa Sheria ambao ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Nimewaita leo kwa ajili ya kuutarifu umma wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa jirani kuhusu Uzinduzi wa Kamati za Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa na Wilaya tarehe **16 Februari, 2026 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja –Dar es Salaam na kufuatiwa na uendeshaji wa Kliniki ya Sheria Bila Malipo kwa wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa Jirani kuanzia tarehe 16 Februari, 2026 hadi 22 Februari, 2026.**

Kamati za Ushauri wa Kisheria za Mikoa na Wilaya zimeanzishwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Huduma za Ushauri wa Kisheria katika Mikoa na Wilaya yaani 'Regional and District Legal Advisory Services (Practice Notes, 2024).
Mwongozo huu umetungwa chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Sura ya 268).

Mwongozo huo pamoja na kamati hizo kwa ngazi ya taifa zilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 21 Machi 2024, katika Mkutano wa Chama cha Mawakili wa Serikali, mkoani Dodoma. Hivyo uzinduzi huu ni kwa ngazi ya Mkoa wa **Dar es Salaam**. Mpaka sasa tumeshazindua na kuendesha kamati hizo na kuendesha Kliniki za Sheria katika mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza, Singida, Manyara na Simiyu.

Kamati hizi, zinapaswa kufanya Kliniki za Sheria bila Malipo katika Mikoa na Wilaya hapa nchini. Lengo ni kusogeza Huduma za Kisheria karibu na Wananchi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya wananchi wanaogopa kwenda kutoa malalamiko yao kwenye ofisi za Serikali na wengine hawana uwezo wa kuzifikia Ofisi hizo kutokana na changamoto za kiuchumi.

Kamati hizi zinalenga kutoa Ushauri wa Kisheria kwa Wananchi, Watumishi wa Umma na Viongozi wa umma ili kutatua changamoto za kisheria zinazojitokeza katika Wilaya zetu na Mkoa kwa jumla.

Sababu za Kuanzishwa Kamati hizo

i) Ongezeko la Notisi au Taarifa za kusudio la kuishitaki Serikali kutokana na mapungufu mbalimbali kutoka kwa Watumishi wa Umma. Matokeo yake Serikali imekuwa ikishitakiwa kutokana na mapungufu hayo,
ii) Ongezeko la malalamiko ya kisheria kutoka kwa wanananchi ambayo yamekuwa yakiwakilishwa kwa viongozi wa ngazi ya kitaifa na mengine kuwasilishwa Ofisini kwangu; na
iii) Kuwepo kwa vitendo vya uvunjifu wa sheria kwa wananchi ambavyo vimekuwa vikiripotiwa katika vyombo vya habari.

Malengo ya kuanzishwa kwa kamati hizi za mikoa na wilaya kwa uchache ni kama ifuatavyo:-

i. Kupunguza mashauri au migogoro dhidi ya Serikali;

ii. Kupunguza malalamiko ya Kisheria kutoka kwa wananchi;

iii. Kutoa elimu ya Sheria kwa umma katika kushughulikia changamoto mbalimbali katika maeneo yao; na

iv. Kupunguza vitendo vya uonevu na vinavyovunja sheria na taratibu.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Nitoe rai kwa wananchi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa jirani kujitokeza kwa wingi siku ya uzinduzi pamoja na kuhudhuria Kliniki ya Sheria **kuanzia tarehe 16 Februari, 2026 hadi 22 Februari 2026**.

Tumeandaa Timu ya Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi yangu na na taasisi zingine, ambao watakuwepo kutoa huduma hiyo bure.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Ninapomalizia taarifa hii, Ninawashukuru sana kwa kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam katika kutoa habari za shughuli zinazofanywa na Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa. Niwaombe mara baada ya kumaliza mkutano huu tufikishe habari hizi kwa Wananchi ili waweze kuitumia Kamati ya Ushauri wa Kisheria ngazi ya Mkoa katika kusuluhisha migogoro inayojitokeza.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**